Swahili | Kiswahili

Australian Government

NATIONAL
CERVICAL SCREENING
PROGRAM
A joint Australian, State and Territory Government Program

# Kuelewa majibu yako ya Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi



## Mwongozo wa kusaidia kuelewa majibu ya Kipimo cha uchunguzi wako wa mlango wa Uzazi.

Daktari wako au muuguzi atazungumza nawe kuhusu majibu ya kipimo chako cha mlango wa uzazi. Pia atakushauri hatua zitakazofuata kutokana na majibu hayo.

Utakapokuwepo na daktari au muuguzi, utakuwa na wakati mzuri kwako kuuliza maswali yoyote au kuwajulisha kama wasiwasi wowote kuhusu majibu yako.

### Je, Kipimo cha Uchunguzi wa mlango wa uzazi huwa kinapima nini?

Kipimo cha uchunguzi wa mlango wa uzazi kinatafuta maambukizi ya virusi viitwavyo papillomavirus ya binadamu (HPV).

HPV ni virusi ambavyo watu wengi huwa navyo maishani bila wao wenyewe kujua kama wanavyo kwani mara nyingi mwenye navyo  haonyeshi dalili yoyote ya kuwa navyo, kwa sababu kawaida hakuna dalili.

Lakini virusi vya HPV vikikaa kwenye miili yetu kwa muda mrefu, vinaweza kusababisha matatizo yanayoweza kusababisha kansa (saratani) ya mlango wa uzazi. Kwa kawaida virusi hivi huweza kuwa kwenye mwili wa mhusika kwa muda wa miaka 10 hadi 15 kabla havijaleta haya madhara.

### Je majibu ya kipimo changu yanamaanisha nini?

Daktari wako au muuguzi atazungumza nawe kuhusu majibu yako ya Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi, na atajibu maswali yoyote utakayokuwa nayo.

Australian Government

NATIONAL CERVICAL SCREENING PROGRAM
A joint Australian, State and Territory Government Program

## Kuelewa majibu ya kipimo chako

Majibu ya kipimo chako yanayoweza kuwa maana tofauti ambazo maana zake zimeelezwa kwenye jedwali lifuatalo:

| | |
|---|---|
| Rudi tena kufanya uchunguzi baada ya miaka 5 | Hakuna virusi vya HPV vilivyogunduliwa katika kipimo chako. Unatakiwa kupima tena baada ya miaka 5. Utakumbushwa nini cha kufanya miezi mitatu (3) kabla ya kipimo kijacho. |
| Rudi kwa mhudumu wako wa afya uchukuliwe kipimo kingine. | Ulichagua kuchukua kipimo chako mwenyewe ambacho kimeonyesha kuna virusi vya HPV. Utashauriwa kurudi kwa daktari wako au muuguzi. Daktari au muuguzi watachukua kipimo kingine kutoka sehemu ya uke wako ambacho pia kina seli za mlango wa uzazi. Haiwezekani kuchukua kipimo hiki peke yako. |
| Rudia kufanya kipimo baada ya miezi 12 | Virusi vya HPV viligunduliwa kwenye kipimo chako, lakini inawezekana mwili wako umeviondoa virusi hivi wenyewe. Ni salama kwako kusubiri miezi 12 kabla ya kupimwa tena. |
| Majibu kutoka maabara hayaridhi. Unapaswa kurudia kufanya tena kipimo cha uchunguzi wa mlango wa uzazi | Maabara hayakuweza kupata jibu kutoka kipimo chako. Hii haimaanishi kuwa kuna kitu kibaya. Fanya miadi ya kufanya kipimo chako tena baada ya wiki 6 hadi 12. |
| Rufaa kwa daktari bingwa | Virusi vya HPV vimegunduliwa katika kipimo chako. Aina hii ya maambukizi ya virusi vya HPV inahitaji vipimo au matibabu ya ziada. Daktari wako au muuguzi atakupa rufaa ya kwenda kumwona daktari bingwa kupata kipimo kingine cha ziada. |

## Maelezo zaidi?

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, zungumza na daktari wako, muuguzi au mfanyakazi wa afya, tembelea www.health.gov.au/NCSP au piga simu kwa **1800 627 701.**

Ili kupata msaada katika lugha yako unaweza kupiga simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS Taifa) kwa **131 450**.
Tembelea www.health.gov.au/NCSP-multicultural ili kupata maelezo yaliyotafsiriwa.